JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA IRINGA

TAARIFA FUPI YA WIKI LA ELIMU MKOA WA IRINGA KATIKA KILELE CHA WIKI LA ELIMU KIMKOA ITAYOFANYIKA MJINI MAFINGA TAREHE 25 MEI, 2017

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

S.L.P. 858,

IRINGA,

Simu: (026) 702021/702715

Nukushi: (026) 2702082/2701888

Barua pepe: *ras@iringa.go.tz*

Tovuti: ***www.iringa.go.tz***

Mei , 2017

TAARIFA FUPI YA WIKI LA ELIMU- MKOA WA IRINGA

1.0. Maendeleo ya Elimu

Mkoa wa Iringa upo mstari wa mbele katika kutoa huduma za jamii ikiwemo Elimu. Zipo Taasisi mbalimbali za Umma na binafsi katika Mkoa ambazo zinajishughulisha na utoaji wa Elimu kuanzia elimu ya awali hadi Vyuo Vikuu.

1.1 Elimu ya Awali na Msingi

Mkoa una jumla ya madarasa ya awali 514 ambapo madarasa 461 yapo katika shule za msingi za Serikali na madarasa 53 yanamilikiwa na taasisi zisizo za Serikali. Aidha, Mkoa una jumla ya shule za msingi 499, kati ya hizo 481 zinamilikiwa na Serikali na 18 zinamilikiwa na Taasisi zisizo za Serikali.

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa madarasa ya awali na shule za Msingi

Halmashauri	Idadi ya shule za Msingi			Shule zenye madarasa ya awali		
	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla
Iringa Manispaa	43	8	51	39	8	47
Iringa	148	1	149	144	35	179
Kilolo	114	-	114	110	0	110
Mufindi	147	2	149	143	3	146
Mafinga Mji	29	7	36	25	7	32
JUMLA	481	18	499	461	53	514

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa, 2017

i) Hali ya Uandikishaji wa Elimu ya Awali, 2017

Mwaka 2017, Mkoa umeandikisha wanafunzi wa elimu ya awali 31,685 ambapo wasichana ni 15,432 na wavulana 16,253. Uandikishaji huu ni sawa na asilimia 90.4 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 35,035.

Jedwali Na: 2: Hali ya uandikishwaji wa Wanafunzi wa darasa la awali hadi kufikia Machi, 2017.

Halmashauri	Waliotarajiwa			Walioandikishwa			%
	Wav	Was	Jml	Wav	Was	Jml	
Iringa MC	2621	2652	5273	2,420	2,312	4732	89.7
Iringa DC	4819	4920	9739	4308	4146	8454	87.0
Kilolo DC	4306	4277	8583	3766	3527	7293	85.0
Mufindi DC	4873	4794	9667	4898	4659	9557	99.0
Mafinga TC	916	857	1773	861	788	1649	93.0
JUMLA	17,535	17,500	35,035	16,253	15,432	31,685	90.4

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, 2017

ii) Hali ya Uandikishaji Darasa la Kwanza, 2017.

Mwaka 2017, Mkoa umeandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza 39,233 ambapo wasichana ni 21,790 na wavulana 17,443. Uandikishaji huu ni sawa na asilimia 110 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 35,538, Uandikishaji huu ni ongezeko la asilimia 9 ikilinganishwa na uandikishaji wa mwaka 2016.

Mwaka 2016, Mkoa uliandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza 35,855 ambapo wasichana ni 17,749 na wavulana 18,106. Ongezeko hili limechangiwa na Mpango wa Serikali ya awamu ya tano wa elimu bila malipo. Hali halisi ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza katika Mkoa imeainishwa katika jedwali Na. 3

Jedwali Na: 3: Hali ya uandikishwaji wa Wanafunzi wa darasa la kwanza mwaka, 2017.

Halmashauri	Waliotarajiwa			Walioandikishwa			%
	Wav	Was	Jml	Wav	Was	Jml	
Iringa Mc	1,656	1,792	**3,448**	2,256	2,238	**4,494**	**130%**
Iringa Dc	5,669	5,551	**11,220**	4,973	4,840	**9,813**	**87%**
Kilolo	4,351	3,936	**8,287**	4,072	3,940	**8,012**	**97%**
Mufindi	4,940	4,929	**9,869**	4,819	9,477	**14,296**	**145%**
Mafinga TC	1,378	1,336	**2,714**	1,323	1,295	**2,618**	**96%**
JUMLA	**17,994**	**17,544**	**35,538**	**17,443**	**21,790**	**39,233**	**110%**

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, 2017

iii) Idadi ya Walimu katika Shule za Msingi za Serikali

Mkoa unahitaji kuwa na walimu 6,240 wa shule za msingi, waliopo ni walimu 5,256 na upungufu ni walimu 984 kwa shule za Serikali.

Jedwali Na.4: Idadi ya walimu wa shule za msingi za serikali mwaka 2017.

HALMASHAURI	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU	ZIADA
IRINGA(M)	709	755	-	46
IRINGA	1725	1272	453	-
KILOLO	1584	1329	255	-
MUFINDI	1745	1474	271	-
MAFINGA TC	477	426	51	-
JUMLA	6240	5256	984	-

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, 2017

iv) Hali ya Miundombinu na Samani katika Shule za Msingi

Mkoa una vyumba vya madarasa 3,961, nyumba za walimu 2,051 matundu ya vyoo 6,380 na madawati 98,283. Mkoa umeendelea kuhakikisha miundombinu muhimu na samani vinapatikana katika shule ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu. Hali ya Miundombinu na samani ni kama inavyoonesha katika Jedwali Na 5.

Jedwali Na. 5: Idadi ya samani na Miundombinu ya shule za Msingi

Na	Aina	Mahitaji	Vilivyopo	Upungufu	Ziada
1	Madarasa	6,027	3,961	2066	-
2	Nyumba za walimu	5,796	2,051	3745	-
3	Matundu ya vyoo	9,073	6,380	2693	-
4	Madawati	88,995	98,283	-	9288

Chanzo: Taarifa kutoka Halmashauri za mkoa wa Iringa, 2017.

Mikakati ya kukabiliana na upungufu wa Miundombinu

Ili kupunguza upungufu wa miundombinu, Mkoa kupitia Halmashauri zake umeendelea kutenga fedha kutoka kwenye mapato yao ya ndani, ruzuku ya Serikali na kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo kuchangia ujenzi wa miundombimu.

v) Matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2016

Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa Mikoa iliyofanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa darasa la saba, kwa mtihani uliofanyika mwezi Septemba, 2016 Mkoa umeshika nafasi ya 3 kati ya Mikoa 26 ya Tanzania Bara ukiwa na ufaulu wa asilimia 82.87 ambapo jumla ya wanafunzi 17,549 (wav. 7,988, was. 9,561) wamechaguliwa na kujiunga na kidato cha kwanza 2017, ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2015 ambapo mkoa ulikuwa nafasi ya 10 ukiwa na ufaulu wa asilimia 73.25.

Ufaulu kimadaraja

Katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi madaraja ya ufaulu ni daraja A, B na C daraja D na E ni wasiofaulu, madaraja ya ufaulu bora ni A na B. Katika mtihani huu jumla ya wanafunzi 17,549 (wav- 7,988, was- 9,561) ndio waliopata daraja A,B na C sawa na asilimia 82.87. Idadi ya wanafunzi waliopata daraja A ni 237(wav 138, was-99) sawa na asilimia 1.1, daraja B ni 3582 (wav-1949, was-1633) sawa na asilimia 16.9, hivyo wenye ufaulu bora(daraja A na B) ni 3,819 (wav-2,087, was-1,732) sawa na asilimia 18 na ufaulu wa wastani (daraja C) ni 13,730 (wav-5,901, was-7,829) sawa na asilimia 64.8. Jedwali Na.6 na Na.7 yameainisha ufaulu kwa kila Halmashauri.

Shule 10 zilizofanya vizuri Kimkoa katika Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi ni St.Dominic Savio, Sipto, Star, Ukombozi, Wilolesi, Ummusalama, St.Charles, Highlands (Iringa Manispaa), Southern Highlands (Mji Mafinga) na Lyalamo(H/W Iringa). Shule 10 za serikali zilizofanya vizuri ni Ukombozi, Wilolesi, Nyumbatatu (Iringa Manispaa) Lyalamo, Lupalama “A”,Isakalilo, Migoli, Msembe (Iringa), Ihefu (Mji Mafinga) na Mlowa (Kilolo). Hali kadhalika zipo Shule 10 zilizofanya vibaya

Kimkoa ambazo ni Chogo, Kitiru, Igomtwa(Mufindi), Kinyali(Iringa), Ulole (Mji Mafinga), Igunga, Ilambo, Idasi, Idegenda na Masisiwe(Kilolo).

Jedwal Na.6: Hali ya ufaulu wa wanafunzi katika mtihani wa kumaliza darasa la saba 2016.

H/W	WALIOFANYA			WALIOFAULU				WASIOFAULU			
	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	%	WAV	WAS	JML	%
Iringa MC	1,618	1,811	3,429	1,414	1,584	2,998	87.43	204	227	431	12.6
Iringa DC	2,448	2,966	5,414	2,122	2,537	4,659	86.05	326	429	755	14.1
Kilolo DC	2,352	2,890	5,242	1,668	2,080	3,748	71.50	684	810	1,494	28.5
Mufindi DC	2,384	3,054	5,438	2,042	2,575	4,617	84.90	342	479	821	15.1
Mafinga TC	788	866	1,654	742	785	1,527	92.32	46	81	127	7.68
MKOA	**9,590**	**11,587**	**21,177**	**7,988**	**9,561**	**17,549**	**82.87**	**1,602**	**2,026**	**3,628**	**17.1**

Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Jedwal Na.7: Ufaulu kimadaraja

NA	HALMASHAURI	WALIOFANYA			A		B		C		D+E		A+B	
		WAV	WAS	JML	JML	%	JML	%	JML	%	JML	%	JML	%
1	MJI MAFINGA	788	866	1654	21	1.3	354	21.4	1152	69.6	127	8	375	22.7
2	IRINGA (M)	1618	1811	3429	169	4.9	935	27.3	1894	55.2	431	13	1,104	32.2
3	IRINGA DC	2448	2966	5414	23	0.4	891	16.5	3745	69.2	755	14	914	16.9
4	MUFINDI	2384	3054	5438	16	0.3	825	15.2	3776	69.4	821	15	841	15.5
5	KILOLO	2352	2890	5242	8	0.2	577	11.0	3163	60.3	1494	29	585	11.2
	MKOA	**9590**	**11587**	**21177**	**237**	**1.1**	**3582**	**16.9**	**13730**	**64.8**	**3628**	**17.1**	**3,819**	**18.0**

Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

1.1 Elimu ya Sekondari

Mkoa una Shule za Sekondari 166 kati ya hizo Shule 107 ni za Serikali na shule 59 zinamilikiwa na Watu binafsi na Mashirika ya Dini. Mchanganuo wa

shule za Sekondari katika kila Halmashauri ni kama inavyooneshwa katika jedwali Na.8.

Jedwali Na.8: Idadi ya Shule za Sekondari

Halmashauri	Shule za Sekondari		
	Serikali	Binafsi	Jumla
Iringa Manispaa	14	15	29
Iringa	28	8	36
Kilolo	24	16	40
Mufindi	33	10	43
Mafinga Mji	8	10	18
Jumla	107	59	166

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa, 2016

i) Idadi ya Walimu katika Shule za Sekondari za Serikali

Mkoa una jumla ya walimu 3,390 kati ya hao Walimu 837 ni Walimu wa sayansi na Walimu 2,553 ni wa masomo ya sanaa. Mkoa una upungufu wa walimu 597 wa sayansi. Idadi ya walimu katika Mkoa ni kama inavyoonesha katika jedwali Na.9:

Jedwali Na.9: Idadi ya Walimu wa Shule za Sekondari za Serikali

HALMASHAURI	ELIMU YA SEKONDARI					
	SAYANSI			SANAA		
	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU	MAHITAJI	WALIOPO	ZIADA
IRINGA(M)	216	145	71	327	522	195
IRINGA	374	188	186	583	753	170
KILOLO	242	152	90	428	518	90
MUFINDI	228	164	64	344	562	218
MAFINGA TC	374	188	186	137	198	61
JUMLA	**1434**	**837**	**597**	**1819**	**2553**	**734**

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa, 2017

ii) Hali ya miundombinu na samani katika shule za sekondari

Mkoa una vyumba vya madarasa 1,412 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya madarasa 1,511. Nyumba za walimu zilizopo ni 559 mahitaji ni nyumba

2880 na matundu ya vyoo yaliyopo ni 2174 ikilinganishwa na mahitaji ya matundu 2679. Mchanganuo umeainishwa katika jedwali Na.10:

Jedwali Na. 10: Hali ya miundombinu na samani shule za sekondari

NA	AINA	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	% UPUNGUFU
1	Madarasa	1,511	1,412	99	6.5
2	Nyumba za walimu	2880	559	2321	80.6
3	Jengo la utawala	107	34	74	69.1
4	Maktaba	107	13	94	87.9
5	Matundu ya vyoo	2679	2174	505	18.9
6	Meza	49518	56866	-	-
7	Viti	49,518	5,555	-	-

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa, 2017

iii) Hali ya Maabara za Sayansi katika Shule za Sekondari

Katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari, jumla ya vyumba vya maabara 321 vinahitajika. Vyumba vinavyoendelea kujengwa ni 144, vyumba 03 vipo kwenye maandalizi ya awali na vyumba vilivyokamilika vyenye samani na vifaa vya kufundishia ni 174, sawa na 54.2%.

iv) Hali ya Ufaulu katika Shule za Sekondari

Ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kimkoa umepanda kutoka 72% mwaka 2014 hadi 89.2% mwaka 2016 hali kadhalika Shule 10 zilizofanya vizuri Kimkoa katika Mtihani wa kidato cha nne ni Mafinga, Bethel, Don Bosco, St. Mary's Ulete, Brooke Bond, Spring valley, Lyanika, St.James, Mufindi wasichana na Magulilwa. Shule 10 za serikali zilizofanya vizuri ni Iringa wasichana, Ifunda ufundi, Kimaiga, Malangali, Idunda, Udekwa, J.J. Mungai, Idodi, Ifwagi na Sadani . Hali kadhalika zipo Shule 10 zilizofanya vibaya Kimkoa ambazo ni Ipeta, Isalavanu, kitowo, kiheka, Kingege, Madege, Nyololo, Itona, Ihanu na Maduma.

Jedwali Na. 11: Ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) mwaka 2014 hadi 2016.

	Mwaka 2014			Mwaka 2015			Mwaka 2016		
	Fanya	Faulu	%	Fanya	Faulu	%	Fanya	Faulu	%
Iringa(M)	1991	1425	72	2764	2167	78	2158	1945	90.1
Iringa	1819	1323	73	3115	2310	74	2209	2002	90.6
Kilolo	1971	1362	69	2595	1846	71	2108	1846	87.6
Mufindi	2,488	1,867	75	2,818	1,772	62	2043	1797	88
Mafinga Tc	-	-	-	1346	1047	78	1080	968	89.6
Mkoa	8,269	5,977	72	12,638	9,142	72	9598	8558	89.2

Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Mkoa wa iringa umeshika nafasi ya 2 kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa ufaulu kwa asilimia 89.2 GPA ya 3.7970 ukilinganisha na mwaka 2015 ambapo Mkoa ulishika nafasi ya tano (5). Idadi ya wanafunzi waliofaulu ni 8,558 (Wav- 4059, Was- 4499) kwa daraja la I – IV kati ya wanafunzi 9,598 (Wav 4501,Was- 5,097) waliofanya mtihani. Wanafunzi walioshindwa ni 1,040 (wav-442,was-598) sawa na asilimia 10.8.

Ufaulu kwa ubora yaani daraja la I-III waliofaulu ni wanafunzi 3406 (wav 2,008 na was 1,398) sawa na asilimia 35.5 tu. Hali hii inaonesha kuwa asilimia 64.5 wamepata ufaulu wa chini au wameshindwa mtihani, ambapo wanafunzi 5,152 (wav-2071,was- 3081) walifaulu kwa daraja la IV sawa na asilimia 53.7.

Matokeo ya mtihani wa Taifa kidato cha nne mwaka 2016 ya watahiniwa wa shule yanaonyesha kuwa ufaulu kitaifa ni asilimia 70.35(wav-73.50%,was-67.34%) ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 67.91 mwaka ya 2015. Kuhusu ufaulu kwa ubora , yaani daraja la I- III, waliofaulu ni asimia 27.6 tu. Hali hiyo inaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 50 ya watahiniwa wamepata ufaulu wa chini au wameshindwa mtihani, ambapo daraja la IV ni asilimia 42.75 na asilimia 29.65 walishindwa mtihani.

Jedwali Na.12 MATOKEO YA MTIHANI WA KITAIFA WA KIDATO CHA NNE

HALMASHAURI	WALIOFANYA			WALIOFAULU				WASIOFAULU				GPA	NAFASI YA UFAULU KITAIFA	
	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	%	WAV	WAS	JML	%		2016	2015
MJI MAFINGA	570	510	1080	517	451	968	89.6	53	59	112	10.4	3.4802		-
IRINGA (M)	928	1230	2158	826	1119	1945	90.1	102	111	213	9.9	3.6824	7	15
MUFINDI	992	1051	2043	886	911	1797	88	106	140	246	12	3.7956		53
IRINGA	1084	1125	2209	1006	996	2002	90.6	78	129	207	9.4	3.8154	23	49
KILOLO	927	1181	2108	824	1022	1846	87.6	103	159	262	12.4	3.9115	36	69
MKOA	**4501**	**5097**	**9598**	**4059**	**4499**	**8558**	**89.2**	**442**	**598**	**1040**	**10.8**	**3.797**	**2**	**5**

Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Jedwali Na.13 UFAULU KIMADARAJA

NA	HALMASHAURI	WALIOFANYA	DARAJA LA 1	%	DARAJA LA 2	%	DARAJA LA 3	%	DARAJA LA 4	%	WALIOSHINDWA	%
1	MJI MAFINGA	1080	96	8.9	112	10.4	234	21.7	526	48.7	112	10.4
2	IRINGA (M)	2158	66	3.1	341	15.8	527	24.4	1011	46.9	213	9.87
3	MUFINDI	2043	34	1.7	225	11.01	390	19.1	1148	56.2	246	12.04
4	IRINGA	2209	62	2.8	252	11.4	409	18.5	1279	57.9	207	9.4
5	KILOLO	2108	18	0.9	191	9.1	449	21.3	1188	56.4	262	12.4
6	**MKOA**	**9598**	**276**	**2.9**	**1121**	**11.7**	**2009**	**20.9**	**5152**	**53.7**	**1040**	**10.8**

Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

1. 2 MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA MWAKA 2016

Mwaka 2016 mkoa ulikuwa na jumla ya Shule 22 zenye watahiniwa 4,040, kati ya shule hizo 15 ni za serikali na 7 zisizo za serikali. Shule tatu za mwanzo zilizofanya vizuri ni Mtera, Changarawe na Ilula. Hali kadhalika shule za tatu za mwisho kati ya shule hizi 22 ni Ifunda ufundi, Highlands na Sadani. Kwa mtihani wa kidato cha sita wanafunzi 3792 kati ya 4040 wamepata daraja la I – III sawa na asilimia 93.8, wanafunzi 177 sawa na asilimia 4.4 wamepata daraja la IV na wanafunzi 71 sawa na asilimia 1.8 wameshindwa mtihani. Jedwali Na.14 limeainisha ufaulu wa kila shule.

Jedwali Na. 14 UFAULU WA KIDATO CHA SITA

NA	HALMASHAURI	SHULE	WALIOFANYA	DARAJA LA 1	%	DARAJA LA 2	%	DARAJA LA 3	%	DARAJA LA 4	%	WALIOSHINDWA	%	GPA
1	IRINGA DC	IFUNDA GIRLS	423	44	10.4	149	35.2	209	49.4	16	3.8	4	1.0	3.396
		IFUNDA TECHNICAL	453	11	2.4	84	18.5	242	53.4	74	16.3	39	8.6	4.045
		ISIMILA	162	7	4.3	106	65.4	49	30.2	0	0	0	0	3.107
		KIWELE	100	10	10.0	63	63	25	25	1	1	1	1	3.053
		MTERA	1	1	100	0	0	0	0	0	0	0	0	2.0
		NYERERE MIGOLI	219	20	9.1	134	61.2	63	28.8	2	0.9	0	0	3.0601
		TOSAMAGANGA	454	29	6.4	142	31.3	242	53.3	30	6.6	10	2.2	3.586
2	IRINGA MC	HIGHLANDS	44	1	2.3	6	13.6	28	63.6	6	13.6	3	6.8	3.7726
		IRINGA GIRLS	329	0	0	132	40.1	154	46.8	17	5.2	5	1.5	3.465
		LUGALO	233	0	0	105	45.1	103	44.2	11	4.7	4	1.7	3.43
		MWEMBETOGWA	179	24	13.4	103	57.5	50	27.9	2	1.1	0	0	3.0047
3	KILOLO	ILULA	94	12	12.8	63	67	19	20.2	0	0	0	0	2.9113
		IMAGE	51	2	3.9	25	49	24	47.1	0	0	0	0	3.2505
		POMERINI	31	2	6.5	20	64.5	9	29	0	0	0	0	3.0281
		UDZUNGWA	74	1	1.4	27	36.5	45	60.8	1	1.4	0	0	3.513
4	MJI MAFINGA	CHANGARAWE	111	34	30.6	74	66.7	3	2.7	0	0	0	0	2.5405
		J.J. MUNGAI	261	32	12.3	128	49	96	36.8	3	1.2	0	0	3.1552
		KAWAWA	129	7	5.4	87	67.4	33	25.6	0	0	0	0	3.0265
		MAFINGA SEMINARY	45	5	11.1	21	46.7	18	40	1	2.2	0	0	3.2185
5	MUFINDI	IGOWOLE	224	24	10.7	127	56.7	71	31.7	1	0.5	1	0.5	3.0997
		MALANGALI	312	26	8.3	222	71.2	63	20.2	0	0	1	0.3	2.9530
		SADANI	151	4	2.7	50	33.1	82	54.3	12	8.0	3	2.0	3.6821
JUMLA KUU			**4040**	**296**	**7.3**	**1868**	**46.2**	**1628**	**40.3**	**177**	**4.4**	**71**	**1.8**	

Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) 2016

1.3 ELIMU MAALUMU, 2017.

Mkoa una shule 1 ya Elimu Maalumu na vitengo 9 na kufanya jumla ya wanafunzi 585 wa Elimu maalum Msingi, kati ya hao wavulana ni 316 na Wasichana ni 269. Elimu maalumu Sekondari, haina shule ya Elimu Maalumu bali ina vitengo 3 vyenye jumla ya wanafunzi 155 kati yao Wavulana ni 89 na Wasichana ni 66. Aidha Mkoa una jumla ya walimu wa elimu Maalumu 138 (wanaume- 63, wanawake- 75)

Utoaji wa elimu maalum katika Mkoa umekuwa ukitolewa kwa mifumo miwili yaani mfumo wa kitengo (intergration) na mfumo jumuishi (inclusive system) lengo la kuwapa elimu wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuwajengea maarifa, Stadi na Mielekeo ya kuwawezesha kushiriki vema katika maendeleo ya sekta kadha wa kadha kama vile elimu, afya na ajira.

1.4 ELIMU YA WATU WAZIMA NA ELIMU NJE YA MFUMO RASMI

Mkoa unaendesha Programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Jumla ya vituo vya MEMKWA ni 18 vyenye jumla ya wanafunzi 338 kati ya hao wavulana ni 205 na Wasichana ni 133. Pia kuna jumla ya vituo 73 vya MUKEJA vinavyoendesha Program mbalimbali. Aidha kuna Program ya Elimu changamani baada ya Elimu ya Msingi (INTERGRATED POST PRIMARY EDUCATION - IPPE) ambapo kuna jumla ya vituo 6 vilivyopo katika Halmashauri 2 yaani Iringa na Mufindi. Mkoa pia una Kituo cha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima chenye jumla ya Wanafunzi 367; wanaume 148 na Wanawake 219. Vituo vya Elimu ya Ufundi Stadi vya serikali vipo 8 ambapo vipo katika Halmashauri za Wilaya ya Kilolo, Iringa na Mufindi. Vituo hivi vinatoa ujuzi mbalimbali kama vile ushonaji, Useremala, Uashi, Ufundi Chuma na Sayansi Kimu.

1.5 Vyuo vilivyopo katika Mkoa wa Iringa

Mkoa wa Iringa una Vyuo vikuu 5 na taasasi za elimu 2 kama ifuatavyo: Chuo Kikuu cha Ruaha (RUCU), Chuo Kikuu cha Iringa (UoI), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa (MUCE) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi pamoja na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Chuo cha VETA.

1. 6 HITIMISHO

Ndugu mgeni rasmi, natumia fursa hii kukushukuru kwa kuungana nasi katika kilele cha maadhimisho haya ya wiki la elimu mkoa wa Iringa. Ninakuhakikishia tumejipanga vizuri kuuletea sifa mkoa wetu kwa kuongeza ubunifu katika utatuzi wa changamoto zinazotukabili ili hatimaye tushike nafasi ya kwanza kitaifa katika utoaji wa elimu bora. Mkoa wa Iringa tunaweza na tunajivunia kuwa na mama mwenye upendo kama wewe.

“Ufundishaji bora wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ni msingi wa maarifa, ujuzi na maendeleo ya elimu katika kufikia uchumi wa viwanda.”

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA